# Radi yasababishia wafugaji umaskin

Ernest Magashi, Mwananchi
emagashi@mwananchi.co.tz

**Bukombe**. Ng'ombe 26 mali ya wakazi sita wa kitongoji cha Sigoba wilayani hapa mkoani Geita wamekufa kwa kupigwa na radi iliyoambatana na mvua.

Mtedaji wa kijiji cha Msonga, Andrew Tungu alisema katika tukio hilo wafugaji; Bundala Saliboko, Joseph Mhangwa na Shikome Mlekwa kila mmoja wamepoteza ng'ombe sita huku Christopher Aloyce akipoteza ng'ombe wanne, Cecilia Sengerema ng'ombe watatu na Ndaki Paul akipoteza ng'ombe mmoja.

**26**

**Idadi ya ng'ombe waliopigwa na radi.**

**6**

**Idadi ya wafugaji waliopoteza mifugo yao.**

Kamanda wa polisi mkoa wa Geita, Mponjoli Mwabulambo alisem tukio hilo lilitokea saa 11:00 jion ya Machi 3 wakati mifugo hiyo iki wa machungani.

Mkuu wa wilaya ya Bukombe, Said Nkumba alitoa pole kwa wafugaji hao na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kuepuka kujikinga mvua chini ya miti mirefu inayovutia radi.

"Nawasihi wananchi kutambua kuwa matukio haya ya radi hayahusiani na imani za kishirikina, nawaonya waganga wa kienyeji na wapiga ramli chonganishi kutowagombanisha wananchi kuhusiana na matukio haya," alisema.

Scanned by CamScanner

# All livestock vaccines to be produced in the country come 2021, declares Ulega

By Guardian Correspondent, Mwanza

THE government has put in place strategies whereby come 2021 vaccines for various livestock diseases will start being produced locally.

This was revealed by the Deputy Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega in Mwanza when he talked with this paper.

He said they have started producing six types of vaccines for livestock diseases to eradicate conning done to herders who buy fake vaccines.

He said the vaccines being produced are for Newcastle disease, mistiss and anthrax among others for both animals and poultry.

Ulega also said the cost to herders for dipping their cattle is 100/- for a single dip while for goats is 50/- whereas pigs are not dipped, they undergo pesticide spray.

Some of the herders in Mwanza region who spoke to this paper at different times, said some of the challenges facing them include the ineffectiveness of many vaccines making them fail to have a solution for their problems.

He said this comes in two ways - low quality vaccines and drugs smuggled into the country by unfaithful business people which have already expired, or those manufactured by rogue factories unknown to the government.

Barandaje said another challenge they face is the lack of extension services - they are not visited by veterinary officials, hence the herders decide to look for themselves for drugs and vaccines for their animals bumping into fraudsters while doing so.

He appealed to the government through Tanzania Food and Drugs Administration (TFDA) to examine the quality of all drugs entering the country, veterinary extension officers to stop staying in their offices.

Another herder, Kundaeli Philipo said it would be a relief to them if the government will implement its strategies to have animal vaccines produced in the country as well as educating them on the better use of the drugs.

Scanned by CamScanner

# Wafugaji washindwa kuuza maziwa baada ya kiwanda kukosa umeme

**Arusha**
**NA LILIAN JOEL**

ZAIDI ya wajasiriamali wa maziwa 500 wa jamii ya kifugaji kutoka kabila la kimaasai, Kata ya Terat, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara wameshindwa kufanyabiashara hiyo kutokana na kutokuwepo kwa umeme katika maeneo yao kwa zaidi ya miaka minne.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa kata hiyo ambao wanapeleka maziwa kwenye kiwanda cha maziwa cha IOPA, Naileji Mollel, alisema uchumi wa wananchi wa kata hiyo umeyumba kutokana na kukosa sehemu ya kuuza maziwa yao.

«Tegemeo letu haswa sisi wanawake katika kukuza uchumi wetu ni kiwanda cha IOPA, lakini kinashindwa kuchukua maziwa yetu kwa sababu kutokana na kutokuwa na umeme hali iliyosababisha kiwanda hiki kufungwa hivyo tunaomba serikali itusaidie kupata umeme ili kiwanda kiweze kufanya kazi,» alieleza.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Martin Sanino, alisema katika kata ya Terati kiwanda hicho ni moja ya kitegea uchumi kwa kina wanawake wanaoishi Wilaya ya Simanjiro na kuiomba serikali kuwatafutia umeme wa uhakika.

Alisema awali kiwanda hicho kilikuwa kinafadhiliwa na watu wa Marekani lakini baada ya ufadhili kufikia kikomo, kiwanda kilishindwa kujiendesha kwa sababu kilikuwa kinatumia jenereta na bajeti ya mafuta ni kubwa.

"Awali kiwanda hiki kilikuwa kinatumia lita 12 kwa saa ikiwa kwa siku ni lita 2,000 hadi 3,000 gharama ambazo ni kubwa na wananchi hawawezi kuzimudu gharama za uendeshaji hali inayosababisha maziwa kumwagwa kwa kuwa hakuna sehemu ya kuyauza,» alibainisha.

Akijibu changamoto hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Umeme Vijijini na Mijini (REA), Julius Kalolo, aliwagakikishia mwishoni mwa mwezi huu kiwanda hicho kitapata umeme pamoja na vijiji vya jirani.

«Serikali ya awamu ya tano itanataka kuwaona wananchi wake wajikwamua kiuchumi hivyo niwambe muendelee kuwa wavumilivu ifikapo mwezi Machi, mtakuwa mmeshapata umeme ili muweze kuendelea na shughuli za kusindika maziwa katika kiwanda hiki,» alieleza.

Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James Ole Millya, ameishukuru bodi ya REA kutembelea eneo hilo na mategemeo yao nikuona changamoto ya umeme maeneo hayo inatatuliwa ili wananchi waendelee na shughuli zao za uzalishaji mali.

«Umeme ukifika katika eneo hili kutawezesha vijana wengi wanaokaa mtaa bila ajira watafungua masaluni nawatafanyakazi katika kuchomelea vyuma na kazi zingine,» alisema.

Scanned by CamScanner

# Mifugo zaidi ya 3,000 yaliwa na Simba Serengeti

**Na Mwandishi Wetu, Mara**

ZAIDI ya mifugo 3, 000 ya wafugaji wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika Wilaya za Tarime, Bunda na Serengeti Mkoa wa Mara wamekufa kwa kuliwa na wanyama wakali wakiwemo Simba na Chui katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Mifugo hiyo iliyoliwa na wanyama hao ni pamoja na Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo ambayo kwa kiasi kikubwa ndio tegemeo kubwa la wafugaji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mikutano iliyohudhuriwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za wilaya hizo wiki hii, wafugaji hao walisema wamebaki masikini kwani baadhi ya familia mifugo yao imekwisha kwa kuliwa na wanyama.

Kutokana na hali hiyo wafugaji hao waliomba msaada wa Serikali ili kunusuru familia zao ikizingatiwa kuwa mifugo hiyo ndio rasilimali pekee wanayoitegemea kuendeshea maisha yao.

Mikutano hiyo ya hadhara ilitishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ambapo iliyofanyika vijiji vya Masanga Wilaya ya Tarime, Nata wilayani Serengeti na Mariwanda wilayani Bunda mkoani Mara.

Wafugaji hao walifafanua kwamba kwa muda mrefu wameteseka na hali hiyo bila kupata msaada wowote kutoka serikalini, hivyo walimuomba Rais John Magufuli awasaidie.

"Tatizo hili ni la siku nyingi lakini hakukuwepo na mkakati wowote wa kuwasaidia hata wawakilishi wa wananchi katika Bunge hawajawahi kuzungumzia tatizo hili ili Serikali iweze kuchukua hatua. Kwa kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi basi Serikali itenge nafasi kwa ajili ya ubunge kurudi kwa wakulima na wafugaji ili waweze kusikia malalamiko yao," alisema mmoja wa wakulima.

Mmoja wa wafugaji wa Kijiji cha Nata, Samweli Mahewa aliomba mwaka huu wa uchaguzi kuwepo nafasi za wabunge wanaotokana na wafugaji waweze kupaza sauti zao bungeni pindi kunapotokea matatizo ya aina hiyo ambayo hayajapata nafasi ya kufikishwa serikalini.

Ofisa Wanyamapori wa Kikosi cha Doria na Kupambana na Ujangili Hifadhi ya Serengeti Kanda ya Bunda, John Msekale, alisema wamekuwa wakichukua hatua za kuwahamisha baadhi ya Simba na kuwapeleka Hifadhi ya Taifa Burigi Chato kama sehemu ya kupunguza tatizo hilo.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mpina alikiri kuwa tatizo kubwa la mifugo kuliwa na wanyama na kwamba Serikali ina kila sababu ya kuingilia kati ili kunusuru hali hiyo kwani idadi ya mifugo iliyouawa na wanyama ni kubwa na hivyo kama Serikali lazima itafute namna bora ya kuwasaidia wananchi hao wasiendelee kupata madhara hayo.

Hivyo Waziri Mpina aliziagiza Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya za Tarime, Serengeti na Bunda, Vikosi vya Doria vya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Halmashauri za Wilaya na Serikali za vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo kuimarisha doria katika vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi hiyo ili kusaidiana na wananchi kupunguza madhara hayo ili wananchi waendelee kuishi kwa amani.

Pia Waziri Mpina aliagiza wataalamu kutoka Wizara nne za Tamisemi, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Mambo ya Ndani ya Nchi kuweka mkakati wa pamoja wa kumaliza tatizo hilo huku akiiwataka wafugaji kujenga mazizi imara ili kujikinga na wanyama wakali pamoja na kujiepusha kuchunga mifugo katika maeneo hatarishi kama sehemu ya kujikinga na athari hizo.

Scanned by CamScanner

# Mifugo 3,000 yaliwa na Simba Mara

**NA MWANDISHI WETU**

ZAIDI ya mifugo 3,000 ya wafugaji wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika wilaya za Tarime, Bunda na Serengeti Mkoa wa Mara wameliwa na wanyama wakali wakiwemo simba na chui katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Mifugo hiyo iliyokufa kwa kuliwa na wanyama hao ni pamoja na ng'ombe, mbuzi na kondoo ambao kwa kiasi kikubwa ndio tegemeo la maisha yao huku wafugaji hao wakimwomba Rais John Magufuli kuwasaidia kuhusiana na suala hilo.

Wafugaji hao wamefikisha kilio hicho kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya hadhara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina iliyofanyika vijiji vya Masanga Wilaya ya Tarime, Nata Wilayani Serengeti na Mariwanda Wilayani Bunda mkoani Mara ambapo walisema kwa muda mrefu wameteseka na hali hiyo bila kupata msaada wowote kutoka serikalini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mikutano hiyo iliyohudhuriwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za wilaya hizo, wafugaji hao walisema kwa sasa wamebaki masikini kwani baadhi ya familia mifugo yao imekwisha kwa kuliwa na wanyama hao na hivyo kuomba msaada wa Serikali ili kunusuru familia zao ikizingatiwa kuwa mifugo hiyo ndio rasilimali pekee wanayoitegemea.

Walisema tatizo hilo ni la siku nyingi lakini hakuna na mkakati wowote wa kuwasaidia wafugaji na kwamba hata wawakilishi wa wananchi katika Bunge hawajawahi kuzungumzia tatizo hilo ili Serikali iweze kuchukua hatua. Wananchi hao waliomba kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi hivyo Serikali itenge nafasi za ubunge kwa kundi la wakulima na wafugaji ili waweze kupata ya kutoa malalamiko yao.

Mmoja wa Wafugaji wa Kijiji cha Nata, Samweli Mahewa, aliomba mwaka huu wa uchaguzi kuwepo nafasi za wabunge wanaotokana na wafugaji ili waweze kupaza sauti zao bungeni pindi kunapotokea matatizo ya aina hiyo.

Ofisa Wanyamapori wa Kikosi cha Doria na Kupambana na Ujangili Hifadhi ya Serengeti Kanda ya Bunda, John Msekale, alisema wamekuwa wakichukua hatua za kuwahamisha baadhi ya simba na kuwapeleka Hifadhi ya Taifa Burigi Chato kama sehemu ya kupunguza tatizo hilo.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mpina alikiri kuwa tatizo kubwa la mifugo kuliwa na wanyama na kwamba Serikali ina kila sababu ya kuingilia kati ili kunusuru hali hiyo kwani idadi ya mifugo iliyouawa na wanyama ni kubwa na hivyo kama Serikali lazima itafute namna bora ya kuwasaidia wananchi hao wasiendelee kupata madhara hayo.

Aliziagiza Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya za Tarime, Serengeti na Bunda, Vikosi vya Doria vya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo kuimarisha [illegible] katika vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi hiyo ili kusaidia wananchi kupunguza madhara hayo.

Waziri Mpina aliagiza wataalamu kutoka Wizara za Tamisemi, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Mambo ya Ndani ya Nchi kuweka mkakati wa pamoja wa kumaliza tatizo hilo huku akiwataka wafugaji kujenga mazizi imara ili kujikinga na wanyama wakali.

Scanned by CamScanner

# Waziri apongeza wazawa uwekezaji sekta ya ngozi

**Na Heckton Chuwa, Moshi**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa ameuongeza uongozi wa kiwanda cha ngozi Himo (Himo Tanneries) kwa uzalishaji unaozingatia kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Bashungwa alitoa pongezi hizo juzi wakati alipotembelea kiwanda hicho, ambapo alishuhudia uzalishaji wa bidhaa za ngozi zinazozalishwa kwa kutumia malighafi ngozi zinazotokana na mifugo ya hapa nchini.

"Kuzalisha bidhaa zinazoongeza thamani ya malighafi zinazopatikana hapa nchini huongeza mapato ya wakulima wetu na pia kuinua uchumi wa Taifa kwa kutumia bidhaa zetu wenyewe, hili hamna budi kupongezwa," alisema.

Adha, alitoa wito wa wawekezaji wengine hapa nchini kujenga mazingira ya uwekezaji utakaolenga malighafi aina mbalimbali zinazopatikana hapa nchini ili wananchi waweze kunufaika kutokana na bidhaa wanazozalisha pamoja na uchumi wa Taifa kukua.

Bashungwa pia aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kuzingatia mpango wa 50-50 unaolenga kuajiri wafanyakazi kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia, mfano amabo alisema ni wa kuigwa na waajiri wengine.

"Pia nwapongeza kwa mipango yenu ya baadaye ambayo mmeainisha hapa ambayo inalenga kujiimarisha kwani kwa kufanya hivyo kiwanda kitaendelea kuweko hivyo kuunga mkono Serikali katika azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Himo Tanneries, Sabas Woiso, alipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuja na sera mpya ya viwanda ambayo alisema inawapa moyo wawekezaji wazalendo.

"Kabla ya kuja kwa sera ya viwanda, wawekezaji wazalendo hatua kuwa na uhakika kama ule tulionao sasa, ila baada ya sera hii kuja tuna uhakika wa kumiliki soko la ndani," alisema.

Woiso alitoa rai kwa Serikali kupitia mamlaka husika kuandaa mpango utakaotoa elimu kwa baadhi ya wafugaji kuachana na tabia ya kuweka alama kwenye mifugo yao maeneo ambayo yataharibu ubora wa ngozi.

"Maeneo mengi tunapata ngozi ambazo ubora wake unakuwa si mzuri kutokana na mifugo kuwekewa alama maeneo yasiyofaa au ngozi kuchunwa vibaya, hili litapuguza idadi ya malighafi za ngozi tunazozitegemea," alisema.

Woiso aliitaja mikoa ambayo hutoa malighafi ngozi zenye ubora kuwa ni ile ya Geita, Mwanza, Simiyu na Kagera.

Katika kuitikia wito wa uwiano wa 50-50 katika kuzingatia jinsia katika kutoa ajira hapa nchini, Woiso alisema kuwa, tayari uongozi wa kiwanda hicho umefikia lengo hilo na kwamba katika idadi ya waajiriwa 100 wa kiwanda hicho 50 ni wanawake na 50 ni wanaume.

Scanned by CamScanner

ugharimu zaidi ya sh. milioni 108.9.
Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa

yamejengwa.

unaokusudiwa

# Wavuvi waomba waruhusiwe kuuza samaki nje ya nchi

**Mwanza**

**NA BALTAZAR MASHAKA**

UMOJA wa Wavuvi wa Tanzania (TAFU) wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuharakisha mchakato wa matumizi ya nyavu pamoja na kuruhusiwa kuuza samaki nje ya nchi.

Ombi hilo limetolewa na wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi kwenye mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji Mkoni Mwanza uliongozwa na Waziri wa Uwekezaji Ofisi ya Waziri Mkuu, Angela Kairuki.

Msemaji wa TAFU, Sijaona James, alisema wizara irekebishe matumizi ya zana za uvuvi na kuharakisha mchakato wa matumizi ya nyavu kama walivyopendekeza na kushauri.

Alisema ni muhimu pia ijielekeze kwenye uzalishaji vifaranga vya samaki pamoja na teknolojia ya utotoleshaji wa vifaranga ambavyo kwa sasa wanaviagiza kutokana nje ya nchi.

Alisema sheria inawazuia wavuvi kuuza samaki kama hawana kiwanda, hivyo aliomba waruhusiwe kuuza samaki popote kama ilivyo kwa ng'ombe.

"Wavuvi tuna wakati mgumu, kwa upande wa masoko sheria hairuhusu mvuvi kuuza samaki nje hadi uwe na kiwanda, ukiangalia suala la tozo zipo zaidi ya 20 ambapo tunaadhibiwa na sheria nyingi ikiwemo ya Uvuvi na Mazingira ya Mwaka 2003," alisema Sijaona.

Naye, Katibu Umoja wa Wafugaji wa Mwanza (UWAU), Suleiman Mathias, alisema wafugaji wa samaki mkoni humu wanakabiliwa na ukosefu wa chakula cha samaki na maeneo ya kufugia hivyo serikali kupitia wizara husika itatue changamoto hizo.

Aidha, Mwakilishi wa Umoja wa Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa mkoani Mwanza (UWAWAMWA), Rehema Mwalugala, alisema ili wazalishe kwa tija na kupata soko la uhakika la maziwa, wizara iwajengee uwezo iwapatie wataalamu.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza kwenye mkutano huo alisema kuwa Sheria ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009, ipo kwenye hatua ya mwisho ya marekebisho makubwa ili kuendana na wakati katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi, kuzitunza na kuzivuna.

Alisema moja ya mikakati wa wizara ni kuona wavuvi wanapata kipato huku zikiendelea na uvunaji wa rasilimali zake na kuwa endelevu ambapo katika mchakato wa kukusanya maoni uliofanyika mwaka 2019, wavuvi walishirikishwa.

Ulenga alisema wamefikia kwenye hatua nzuri na za mwisho za marekebisho ya sheria hiyo ya uvuvi na kanuni zake ndio sababu ya kuwapa matumaini wadau wa sekta ya uvuvi.

Scanned by CamScanner

# Wavuvi Kalambo washauriwa kujiunga vikundi

**Na Israel Mwaisaka, Kalambo**

WAVUVI wa Ziwa Tanganyika wilayani Kalambo Mkoa wa Rukwa, wameshauriwa kujiunga na vikundi vitakavyowasaidia kupata mikopo, hali itakayowawezesha kununua zana za uvuvi wa kisasa na hivyo kuacha kujihusisha na vitendo vya uvuvi haramu.

Wito huo uliotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Msongela Paleja wakati akikagua Soko la Kimataifa la Samaki lililojengwa katika Kijiji cha Kasanga wa Ziwa Tanganyika uliopo katika halmashauri hiyo, una wavuvi 1,000 na kati yao 700 ndiyo wenye zana za uvuvi na wanafanya shughuli hizo kila siku.

Mkurugenzi huyo alisema, changamoto kubwa inayowakabili wavuvi hao ni kutokuwa na zana bora na zinazoruhusiwa kisheria kufanya kazi hiyo, kitendo kinachosababisha wengi wao kukamatwa mara kwa mara kwa kutuhumiwa kuwa ni wavuvi haramu.

Alisema hali hiyo, imekuwa ikiwatokea kutokana na kukosa mitaji ya kununulia zana zinazokubalika kisheria, hivyo kupata sifa za kukopesheka na kuweza kununua zana zinazotakiwa na kuepukana na changamoto wanazokabiliana nazo mara kwa mara.

Paleja alisema hivi sasa wamepata soko hilo, baada ya serikali kusikia kilio chao na kuamua kuwajengea soko la kisasa na la kimataifa, hivyo wa wahakikishe wanalitumia ipasavyo kwani linatarajiwa kuzinduliwa siku chache zijazo kilichobaki ni kuboresha hali zao za kiuchumi kutokana na kuwepo kwa soko hilo.

Mmoja wa wavuvi hao, Skeva Sinyangwe alishukuru serikali wa soko la uhakika la mazao ya uvuvi, kitendo kilichokuwa kikiwalazimu kupeleka mazao hayo katika nchi jirani za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambapo walikuwa wakikutana na changamoto kubwa zaidi hali iliyokuwa ikisababisha mitaji yao kutokukua.

Alisema pia suala la usalama wao na biashara zao, likuwa ni tatizo kubwa kwani baadhi yao wamepoteza mitaji na mali zao kutokana na vitendo vya ujambazi na uharamia, vinavyofanyika majini hali ambayo kwa sasa itabaki historia, kwani watakuwa wakifanya biashara hiyo wakiwa ndani ya nchi na kufaidi rasilimali

# Mghwira aipa somo jamii ya wafugaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ameitaka jamii ya wafugaji katika vijiji vya Tindigani, Mtakuja na Sanya Station, Wilaya ya Hai kufikiria kuuza mifugo michache na kujenga makazi bora badala ya kuendelea kuishi kwenye nyumba za tembe na tope.

Mghwira alitaka mabadiliko hayo juzi, alipoongozana na kamati yake ya ulinzi na usalama kwenda kukagua nyumba 43 kwenye vijiji hivyo, zilizobomoka na nyingine kuanguka kabisa kutokana na mvua za masika zilizonyesha juzi kwa saa kadhaa zikiambatana na upepo.

"Haina maana kuwa na mifugo mingi wakati unaishi maisha duni, badilikeni fugeni mifugo michache yenye tija ili mjenge nyumba bora mwondokane na kuishi maisha duni.

Zaidi Mghwira alisisitiza kuwa: "Mkiangalia nyumba nyingi zilizobomoka ni nyumba zilizojengwa kwa matope, hii ni hatari katika nyumba ya Alex Sabore ambaye ana mtoto wa miaka minne aliangukiwa na nyumba na sasa yupo ICU (chumba cha uangalizi maalum) cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC."

Akiwa katika Kata ya Kia, Diwani wa Kata hiyo, Yohana Laizer, alimweleza mkuu huyo wa mkoa kwamba kwa sasa wananchi hao wamejihifadhi kwa majirani zao, wakati wakiendelea kukarabati nyumba zao.

Katika Kijiji cha Sanya Station, watu 34 hadi kufikia sasa hawana makazi kutokana na nyumba zao kubomolewa na mvua.

Wakati katika Kijiji cha Tindigani, nyumba nane zimeharibiwa vibaya na Mtakuja nyumba moja imeanguka, huku pia mvua hiyo ikiacha hasara ya kung'oa miti kuua mifugo.

Scanned by CamScanner